

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

## MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 17 mwezi 02 *Abdalla* 2021/2022

### KATI YA

Chuo cha Ufundı Stadi (na Huduma) cha VETA - DSM, S.L.P. 40274,  
DAP ES SALAAM ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya  
Ufundı Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana  
kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

FRANSIS NGEZA S.L.P. \_\_\_\_\_, PANGANI - TANGA  
(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundı") kwa upande mwengine

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundı Stadi cha Wilaya ya  
PANGANI ;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za  
nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundı Stadi cha Wilaya ya PANGANI ;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Fundı kwa ajili ya kazi ya  
KUMALIZIA KUPIGA PLASTER MATENGU TA. 1 JENGO LA STORE JENGO LA  
JIKO, BWENI LA WAVULANA, PAMOJA NA KUJENGA MATUNGULIZI KARIBWE  
NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundı nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo  
wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinayoonesha namna kazi itakavyofanyika;

HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

### 1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 4,000,000/-, Fundı  
atafanya kazi ya KUJENGA NA KUPIGA PLASTER kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.  
Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundı"

## 2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

## 3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

- (a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
- (b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundii;
- (c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundii;
- (d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80:30% ya Gharama ya Ufundii;
- (e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundii;na
- (f) Baada ya kukamilika kwa "Muda wa matazamio":5% ya Gharama ya Ufundii.

## 4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI.

- (a) Fundi atakabidhiwa eneo la tarehe 18 mwezi 02 <sup>taratu</sup> ~~2021~~ <sup>2022</sup> au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.

- (b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 10 toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.

- (c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

## 5. WAJIBU WA FUNDI

Fundi atakuwa na wajibu ufuatao: -

### KUJENGA NA KUPIGA

- (a) Kujenga PLASTER na kukamilisha ujenzi kama inavyoonekana katika Michoro pamoja na Mchanganuo wa Yifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) sambamba na maelekezo ya Mwajiri;

- (b) Kumpatia Mwajiri ratiba ya kazi (*work programme*) ndani ya siku 7 tangu tarehe ya kusaini Mkataba huu ili kupata kibali cha Mwajiri.

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA  
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA

Jina:

Joseph Mwande

Saini:

Wadhifa:

Mumu wa Chuo

Tarehe:

17/02/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina:

JUMA I. MBALA

Saini:

MBALA

Wadhifa:

MUSIMAMIZI WA MPELE

Tarehe:

17/02/2022

#### IMESAINIWA NA FUNDI

Mbele ya

Jina:

FRANCIS S. NGOTI

Saini:

FSGT:

Wadhifa:

Fundi

Tarehe:

17/02/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina:

THAPPI S. CHUMA

Saini:

WL:

Wadhifa:

P/ierch.

Tarehe:

17/02/2022